



ARUSHA MEAT COMPANY LTD.

P.O.BOX 14167

ARUSHA

TANZANIA

TEL: +255272970304

Mob: +255734026767

E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

Kumb Na: AMCL/SEC/051/11

13/05/2024

ZABUNI YA ULINZI

1. Arusha meat Co.ltd kupitia kamati ya Manunuzi inakusudia kufanya mchakato kwa ajili ya kupata kampuni ya ulinzi.
2. Kampuni zote za ulinzi zenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili ofisi ya manunuzi Arusha Meat Co. Ltd na kutembelea eneo la kazi Arusha Meat Co.ltd
3. Hivyo basi Meneja Mkuu wa Arusha Meat Arusha Meat Co. Ltd kupitia Kamati ya manunuzi anatangaza zabuni ya ulinzi.

Majukumu katika kazi ni kama ifuatavyo;

- a) Kukagua magari na mizigo yote inayoingia na kutoka dani ya kampuni
 - b) Kulinda mali za kampuni na wafanyakazi wake.
 - c) Kutunza kumbukumbu za mali za kampuni na wateja ikiwa ni pamoja na kuhakiki na kurekodi mali na vifaa vinavyoingia na Kutoka nje ya kampuni.
 - d) Kutoa taarifa za kiusalama juu ya usalama wa mali za kampuni pale inapohitajika.
 - e) Kuzuia uhalifu kutokea kwa kuchukua hatua za tahadhari na kuchunguza kwa umakini tabia zinazotiliwa shaka na kuwasilisha katika mamlaka husika.
4. Sifa za kampuni ya ulinzi inayotakiwa
- a) Iwe na uzoefu usio pungua miaka mitano mfululizo katika kazi kama ilivyo ainishwa hapo juu.
 - b) Iwe na namba ya mlipa kodi kutoka mamlaka ya mapato Tanzania (Tax Identification Number).
 - c) Iwe na mtaji wa kutosha kwa maana ya rasilimali watu na vitendea kazi muhimu.
 - d) Iwe na akaunti ya benki.
 - e) Iwe na Leseni halali ya biashara.
 - f) Iwe na Leseni ya silaha za moto inayotolewa na mamlaka husika.

- g) Iwe na cheti halali cha usajili wa mahali pa kazi.
- h) Iwe na orodha ya mikataba mitatu ya kazi ya ulinzi aliyopata hivi karibuni (2023/2024) ikiwa ni pamoja na majina na anwani za wateja kwa ajili ya kuthibitishwa.
- i) Iwe na kibali cha uthibitisho wa kutoa huduma ya ulinzi kinachotolewa na jeshi la polisi.
- j) Iwe na leseni ya radio call.
- k) Taarifa ya fedha iliyokaguliwa angalau miaka miwili ya hivi karibuni.
- l) Taarifa ya akaunti ya benki ya miezi mitatu ya hivi karibuni.

NOTE:

- Wawakilishi wa Kampuni zote zilizoomba zabuni ya Ulinzi wawepo siku ya ufunguzi ili kufuatilia kwa ukaribu hatua zote za mchakato wa ufunguzi wa zabuni zilizowasilishwa.
- Wazabuni wenye nia na uwezo wawasilishe maombi yao katika Masijala ya ARUSHA MEAT CO.LTD Kabla ya muda wa kufunga zoezi la upokeaji maombi ya zabuni.
- Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 28/05/2024 siku ya jumanne saa nne kamili asubuhi (04:00 Asubuhi) na zitafunguliwa tarehe 28/05/2024 saa nne na dakika Moja asubuhi (04:01 Asubuhi) katika Ofisi za Arusha Meat. Ltd.

Maombi yote yatumwe kupitia anuani ifuatayo:

Meneja Mkuu,

Arusha Meat Co. Ltd,

S.L.P. 14167,

Arusha.

Maombi yote yafungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri (seal) na juu ya bahasha iandikwe "Zabuni ya ulinzi Arusha Meat Company Ltd - AMCL/SEC/051/11.

Karibuni wote,


STEPHEN L SULTAN
MENEJA MKUU
ARUSHA MEAT COMPANY LTD

